Miti inayogeuka mawe Selous,kivutio kipya cha utalii

Na Albano Midelo

PORI la akiba la Selous ni moja kati ya hifadhi zenye utajiri wa vivutio adimu vya utalii ambavyo vinaweza kuliingizia taifa fedha nyingi za kigeni na kuongeza pato la taifa.



Sekta ya utalii hivi sasa inaongoza kwa kuliingizia Taifa mapato ambapo inaingiza dola za Marekani bilioni mbili kwa mwaka.

Selous ni pori la akiba lenye ukubwa wa kilometa za mraba 50,000 likijumuisha maeneo ya ardhi oevu,misitu ya miombo,tambarare ,nyasi za kuvutia,maziwa na mito inayotiririka na kuwa kivutio.

Pori la akiba la Selous lilianzishwa mwaka 1896 na wajerumani likiwa ni pori la kwanza kutengwa kwa ajili ya

uhifadhi wa wanyamapori katika Bara la Afrika na la pili duniani kwa ukubwa baada ya hifadhi ya pori la Marekani ambalo linaitwa Yellowstone.

Umaarufu wa Selous si katika wanyama pekee ambao ndiyo kivutio kikubwa cha utalii wa uwindaji,utafiti umebaini kuwa katika eneo la Selous kuna utajiri mkubwa wa maliasili ya mimea ambayo ikitambuliwa na kutangazwa inaweza kuwa kivutio adimu na cha kipekee cha kitalii.

Utafiti uliofanywa katika pori hilo na wataalam kutoka nje ya nchi kwa kushirikiana na wataalam wa wizara ya maliasili na utalii umebaini kupatikana zaidi ya aina(species) 2100 za mimea zilizotambuliwa na wanasayansi ikiwemo aina 600 za miti ambayo haipatikani sehemu nyingine duniani.

Mkurugenzi Mstaafu wa Uhifadhi ambaye pia amewahi kuwa Mkuu wa Chuo cha Wanyamapori Kanda ya

Likuyuseka katika Pori la Selous Ngwatura Ndunguru anaitaja Moja ya jamii ya miti ambayo haijafahamika na kutangazwa ipasavyo kuwa ni magogo ya miti iliyogeuka mawe ambayo kitaalam inaitwa *fossilized tree trucks* .

Masalio ya magogo hayo bado yanaonekana katika baadhi ya maeneo ya ndani na nje ya hifadhi ya Selous katika vijiji vya Mpurakacheche na Mbarang'andu Wilaya ya Namtumbo Mkoa wa Ruvuma.

Hata hivyo Ngwatura anasisitiza kuwa mawe hayo yakitangazwa kwenye vyombo vya habari,mamia ya watalii wanaweza kwenda katika Wilaya hiyo kuona kivutio hicho kipya na cha kipekee hivyo kuingiza mapato na fedha za kigeni ambazo zitasaidia kuinua uchumi wa Taifa.

Moja ya maeneo ambayo inapatikana miti iliyogeuka mawe katika pori la akiba la Selous ni Kanda ya Kalulu ambayo ipo upande wa kusini mwa pori hilo.

Eneo hilo ambalo lipo umbali wa kilometa 96 kutoka mjini Tunduru linakadiriwa kuwa na kilometa za mraba 6148.4.Kijiji cha Kalulu kipo umbali wa kilometa 230 kutoka Makao Makuu ya Mkoa wa Ruvuma Songea.

Kanda ya Kusini ya pori la Selous yaani Kalulu kwa mujibu wa Mhifadhi Kabanda Ismail ina umaarufu wa eneo lenye miti iliyogeuka kuwa mawe.Hali hiyo inatokana na hali ya kijiolojia inayotokea kwa mamilioni ya miaka na kuyageuza masalia ya miti kuwa mawe.

Mkurugenzi Mstaafu wa Uhifadhi Ngwatura Ndunguru anasema miti ambayo imegeuka mawe inapatikana katika eneo lililopo katikati ya Lipembe na Mbarang'andu ndani ya pori la Selous na kwamba katika hali ya kawaida sio rahisi kuamini kuwa mti unaweza kugeuka jiwe.

"Utafiti wa kiikolojia umebaini kuwepo kwa mkaa wa mawe ambao asili yake ni miti.Ukitembelea eneo hilo la mawe ya

asili ya miti,utabaini picha halisi ya miti yaani matawi na maeneo ambayo matawi yake yalidondoka ambapo alama zake bado zipo hadi sasa hali ambayo inathibitisha ukweli wa kisayansi",anasisitiza Mhifadhi Ngwatura.

Historia inaonesha kuwa maeneo yote ambayo miti imegeuka mawe hayakaliwi na watu wengi wala hakuna mtu anayeingia ndani ya eneo hilo hali iliyosababisha maeneo hayo kubakia katika hali yake ya asili ya kijiolojia ya kutoharibiwa kutokana na shughuli mbalimbali za kibinadamu.

Mhifadhi Imanuel Nyanda anasisitiza kuwa kugundulika kwa aina hiyo mpya ya utalii ndani ya pori la Selous ni vema Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kuyalinda,kuyaendeleza kuyahifadhi na kuyatangaza maeneo hayo ili watalii wa ndani na nje ya nchi waweze kumiminika na kwenda kufanya utafiti na kujifunza zaidi.



Utafiti wa kisayansi unaonesha kuwa kivutio cha namna hii huwezi kukipata katika sehemu nyingine yeyote kusini mwa Jangwa la Sahara zaidi ya pori la Selous.

Kutokana na pori hilo kuwa na rasilimali adimu za asili, Shirika la Umoja wa Mataifa la Sayansi,Elimu na

Utamaduni (UNESCO) liliamua kulitangaza pori la Selous kuwa ni urithi wa Dunia tangu mwaka 1980.

“Kinachotakiwa kwa serikali ni kutoruhusu shughuli za kibinadamu kama uchimbaji wa madini na uwindaji haramu kufanyika ndani ya pori hili kwa sababu kunaweza kuathiri kivutio hiki adimu na vivutio vingine ”,anasema Mhifadhi Ngwatura.

Hata hivyo utafiti wa kimataifa umebaini miti inayogeuka mawe iliyopo pori la Selous Tanzania inapatikana pia kaskazini mwa Afrika katika nchi za Misri,Libya na Algeria,pia miti hiyo inapatikana katika nchi ya Ugiriki na Marekani.

Tovuti ya Kimataifa ya **www.temehu.com** imeandika masalio ya magogo yalioishi mamilioni ya miaka na kugeuka mawe yanapatikana katika eneo la Fezzan kusini magharibi mwa nchi ya Libya.

Kulingana na tovuti hiyo masalio ya vipande vya magogo vilivyogeuka mawe yamegundulika kwenye msitu uliopo katika eneo la kati ya Ubari-Awaynat karibu na mto Raha nchini Libya.

Imebainika msitu huo una magogo makubwa yenye urefu wa mita 20 na kwamba magogo ya miti hiyo kabla ya kugeuka mawe yalichukua kati ya miaka milioni 90 hadi 95.

Makala ilioandikwa na Profesa Noel Boaz wa Sayansi ya Mimea kwenye tovuti hiyo imezitaja nchi ambazo zina magogo yalioishi mamilioni ya miaka na hatimaye kugeuka mawe kutoka katika misitu na hifadhi za Taifa.

Kwa mujibu wa Profesa Boaz maeneo hayo ni msitu wa Salah nchini Algeria,nchi ya Misri ambako kuna magogo yalioishi karibu miaka milioni 35 iliyopita kabla ya kugeuka mawe,nchini Marekani katika hifadhi ya Taifa ya Arizona kuna magogo yaliogeuka mawe na eneo la Lesbos katika nchi ya Ugiriki.

Ugunduzi wa miti iliyogeuka mawe katika pori la Selous ni changamoto kwa serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii kuhifadhi miti iliyogeuka mawe katika Makumbusho ya Taifa ambapo katika Mkoa wa Ruvuma kuna Makumbusho ya Taifa ya majimaji ambako mawe hayo

yanaweza kuhifadhiwa na kuvutia watalii wengi wa ndani na nje.

Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa ya Majimaji Balthazar Nyamusya ameahidi ofisi ya Makumbusho ya Taifa ya Majimaji kufuatilia mawe hayo ili kuyahifadhi katika Makumbusho kama rasilimali muhimu ya Taifa.

Nyamusya anasisitiza kuwa Katika Makumbusho ya Taifa ya Majimaji kuna kumbukumbu adimu zikiwemo silaha halisi walizotumia mashujaa wa vita vya majimaji mwaka 1905,hivyo iwapo miti iliyogeuka mawe itawekwa katika Makumbusho hayo itawarahisishia watalii na wasomi kufika kuangalia na kujifunza.

Albano Midelo ni Mchangiaji wa Gazeti hili,anapatikana kwa simu 0784765917,baruapepe albano.midelo@gmail.com